Al-Islam.org
Ahlul Bayt Digital Islamic Library Project
Published on *Al-Islam.org* (https://www.al-islam.org)

Mtazamo wa Uislamu

Mungu alimtuma Yesu kwa Wayahudi kwa sababu waliiacha ibada ya Mwenyezi Mungu kwa madai na visingizio kwamba wanafuata sherehe na uchambuzi wa kina wa sheria. Vitabu 63 vya Talmud – ambavyo ni tafsiri na uchambuzi wa sheria ya kiyahudi – ni uthibitisho juu ya jambo hili. Wayahudi waliamini kwamba wokovu unapatikana kwa kutii sheria ya Mungu.

Yesu alitumwa katika jitihada za kuwaelewesha kwamba vitendo vizuri peke yake sio mwisho wa mambo yote bali walitakiwa pia kumuamini Mwenyezi Mungu. Yesu alihimiza tena na tena kwamba "ibada tupu bila imani thabiti", si jambo lililotakiwa na Mungu kutoka kwao bali lililokuwa likitakiwa ilikuwa ni kufuata sheria zilizomo katika maandiko matakatifu "kwa dhati, uchaji Mungu na kumhofu Mwenyezi Mungu kwa dhati".1 Hili ndilo jambo ambalo Yesu alilifundisha bila kuchoka lakini kwa bahati mbaya, leo hii haya sio mafundisho ambayo Ukristo unasimamia utekelezaji wake ule ujumbe wa Yesu:

"Amri kuu kuliko zote ni, sikieni, Enyi Israel; Bwana Mungu wetu ni Mungu mmoja".

Unaopatikana katika Marko 12:29, si chochote ila ni maandishi tu katika karatasi Paulo alimpachika Yesu uungu, kisha akaandaa masharti ya uokovu kwamba kilichotakiwa ni imani peke yake juu ya Yesu kwamba alikufa kwa ajili ya dhambi za wanadamu. Utii wa sheria ya Mwenyezi Mungu ulitupiliwa mbali na ukaitwa kuwa ni "Laana". Qur'an imeliweka jambo hili wazi kabisa. Imetaja masharti ya uokovu kuwa ni mawili, kumwamini Mwenyezi Mungu Mmoja na kutii sheria zake.2 *"**Kwa wale ambao wameamini na wakafanya vitendo vizuri Mwenyezi Mungu amewaahidi msamaha na malipo makubwa**". (Qur'an 5:9*)

1. What Everyone Should Know About Islam and Muslims, p. 180. (Mambo yampasayo kila mmoja kuyajua juu ya Uislamu na Waislamu, uk. 180.)
2. (Qur'an 5:9)

Source URL:
https://www.al-islam.org/uchunguzi-makini-juu-ya-ukristo-barbara-brown/mtazamo-wa-uislamu